# Msimamo wa Mtandao wa Wanawake, Katiba, Uchaguzi na Uongozi kuhusu Mapendekezo ya Kikosi Kazi katika Ushiriki wa Wanawake katika Demokrasia ya Vyama Vingi.

## 1.0 UTANGULIZI

Sisi Wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi ambao ni muunganiko wa asasi za kiraia zaidi ya 200 ulioanzishwa mwaka 2011 wakati Rais wa awamu ya Nne, Mh. Jakaya Kikwete alipotamka nia ya kuanza mchakato wa kutayarisha Katiba Mpya. Mtandao huu unao dhaminiwa na Mfuko wa Udhamini wa Wanawake Tanzania, uliitisha kongamano la kutafakari jinsi ya kuwezesha kuingiza masuala ya jinsia katika Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kikao cha Mtandao cha kwanza, Wanamtandao walikubaliana kujenga nguvu za pamoja na kuwa na ajenda moja katika mchakato wote wa kutayarisha Katiba mpya. Mtandao huu, ulibainisha masuala 12 ya kuingiza katika Katiba mpya, huku wakikubaliana kwa sauti moja kwamba wanawake wa Tanzania wanataka Katiba yenye mrengo wa jinsia. Kati ya misingi 12 ya kikatiba waliyokubaliana, ushiriki wa wanawake katika uongozi kwa asili 50/50 ulikuwa mojawapo.

Ke storia ya madai ya usawa wa jinsia katika ngazi za maamuzi ni ajenda ya muda mrefu ya wanaharakati watetezi wa haki za wanawake Tanzania tangu tupate uhuru wakati waasisi wa utetezi huo Bibi Titi Muhamed na viongozi wengine wa chama Tawala cha TANU walipohoji kukosekana kwa wanawake kwenye serikali ya awamu ya kwanza chini ya Mwl Julius Kambarage Nyerere. Hadi leo hii, haki ya kushiriki katika ngazi ya maamuzi imekuwa ni ajenda muhimu katika harakati za utetezi wa haki za wanawake. Kimsingi, haki ya usawa wa ushiriki imebainishwa katika Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kifungu cha 21 kinachotamka wazi kwamba “kila *raia wa Tanzania ana haki sawa ya kushiriki katika utawala wa nchi aidha moja kwa moja au kwa uwakilishi*”. Dira ya Taifa ya 2025 imekiri dhamira ya kutokomea kwa aina zozote za ubaguzi ifikapo mwaka 2025 . Vile vile haki Tanzania imeridhia mikataba, matamko na itifaki za kimataifa ikiwa ni pamoja na; Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu (1948) Azimio la Kimataifa kuhusu Haki za Kiraia na Kisiasa (1966) Mkataba Kuhusu Haki za Kisiasa za Wanawake (1952), Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW) (1979) Mkataba huu unazitaka nchi wanachama kuchukua hatua za makusudi kurekebisha tofauti ya jinsia katika uongozi. Azimio la Beijing la mwaka 1995, Mpango Kazi wa Beijing Ulibainisha maeneo 12 ya Kipaumbele katika utekelezaji, ambapo Tanzania ilichagua maeneo manne moja likiwa ushiriki wa wanawake katika uongozi wa Siasa na Ngazi zote za Maamuzi. Misingi na Miongozo inayoongoza uchaguzi wa kidemokrasia katika nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Africa (Declaration of PrincipalsGoverning Democratic Elections in Africa (2022), Sera ya Jinsia Ya AU 2009), Itifaki ya Mkataba wa Afrika juu ya haki za wanawake (Protocol to the African Charter on Human and Peoples')

Mikataba, itifaki, maagano, na Matamko haya yametafsiriwa katika Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kifungu cha 12 (1&2) kimebainisha misingi ya usawa ambayo yataongoza sheria na sera zote za nchi, ambapo kifungu cha 21 kinatamka wazi kwamba

> "Kila *raia wa Tanzania ana haki sawa ya kushiriki katika utawala wa nchi aidha moja kwa moja au kwa uwakilishi*", na kifungu kidogo cha Ibara hii kinasema "kila raia ana haki ya kushiriki katika uongozi wa taifa hili, aidha moja kwa moja au kwa kutumia wawakilishi.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1985, iliingiza kifungu cha kuwezesha ongezeko la wanawake kwa kupitia viti Maalum kwa asili mia 15, ambapo maboresho ya katiba hii ya mwaka 2000 iliongeza kiwango cha viti maalum kuwa asili mia 20 na kufikia asili mia 30 katika maboresho ya mwaka 2005. Pamoja na hatua hizi, bado pengo la jinsia linajitokeza katika ngazi zote za maamuzi, ikiwa ni pamoja na ushiriki wao katika vyombo vya uwakilishi, katika teuzi mbalimbali, na katika uongozi wa mashirika ya umma na hata yale ya binafsi. .

Pamoja na misingi hii iliyobainishwa kwenye Sheria mama ya nchi na kuainishwa kwenye dira ya Taifa 2025, Bado Pengo la jinsia katika Nyanja ya uongozi limeendelea kuwepo.

### 1.1 Hali Halisi ya Ushiriki wa Wanawake katika Uongozi

Ushiriki wa wanawake katika chaguzi mbalimbali hapa nchini unonyesha kwamba, idadi ya wanawake wanaoingia Bungeni imeongezeka kutoka 101 mwaka 2005 na kufikia 145, mwaka 2015. Hata hivyo ongezeko hili limetokana na uwakilishi kwa kupitia viti maalum. Kwa mfano kwenye Bunge la 2005, wanawake kutoka majimbo walikuwa 20, ambapo wa viti maalum walikuwa 75, walioteuliwa na Rais walikuwa 4, wawakilishi wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar 2, Jumla 101. Uchaguzi wa 2010, wabunge wanawake kutoka majimbo walikuwa 21, kupitia viti maalum 102, walioteuliwa na Rais 5, kutoka Baraza la Wawakilishi 2, Jumla kuu 130. Katika uchaguzi wa 2015, jumla ya wanawake Wabunge ilifikia 145 au asili mia 37, ikiwa waliotoka kwenye majimbo ilikuwa 25, viti maalum 113, walioteuliwa na Rais 3, na wawili kutoka Baraza la Wawakilishi Z'bar.

Ingawaje idadi ya uwakilishi katika ngazi hii imeongezeka, walio wengi wao wanapitia viti maalum. Ripoti za wachunguzi wa Uchaguzi ya mwaka 2015 ilikiri, kama hatua za makusudi hazitachukuliwa za kurekebisha uwanda wa ushindani, basi italichukua Taifa letu miaka 165 au chaguzi 33 kufikia usawa wa jinsia katika uwanda wa ushindani (Ripoti ya CEMOT 2015)

Katika ngazi nyingine za uongozi ushiriki wa wanawake bado haujafikia lengo la 50/50 kama lilivyoainishwa kwenye mkataba wa AU na kuthibitishwa na Chama Tawala CCM mwaka 2015. Kwa mfano katika kipindi kutoka 2005 hadi 2010, wanawake katika ngazi ya uwaziri walikuwa asili mia 35 kutoka miaka ya 2014-2015, lakini kiwango hiki kikashuka na kufikia asili mia 17

mwaka 2016. Kwa sasa hivi, kiwango hicho kimepanda kufikia asili mia 36. Hata hivyo katika ngazi ya Manaibu mawaziri, kuna wanawake 5 tu au asili mia 20 tu ya Manaibu Mawaziri wote.

Kwenye ngazi ya makatibu wakuu, na manaibu makatibu wakuu, kuna wanawake 4 tu sawa na 15.3 %, kati ya makatibu 26 na wanawake 6 tu kati ya manaibu 30 sawa na 20% tu. Katika ngazi ya uongozi wa Mkoa, idadi ya sasa hivi wanawake wako wanane (8) tu kati ya Wakuu wa Mikoa 26, sawa na 30.7% (Kati ya wakuu wa wilaya 140, wanawake ni 40 tu sawa na asili mia 28.5% (ibid,).

Akielezea changamoto zinazo likabili Taifa kufikia 50/50, Rais Samia Suluhu Hassan, kwenye mahojiano na mwanahabari Anold Kayanda wa Idhaa ya Umoja wa Mataifa September 2021 kuhusu suala la 50/50 la usawa wa jinsia alisema,

> "---, safari ni ndefu lakini mwelekeo upo. Na mwelekeo upo sio kwamba mimi nimeingia lakini kama tutakumbuka ukitazama kuanzia awamu ya nne tumekuwa tukielekeza kufikia usawa wa kijinsia. Ni awamu ya nne ile ile pia ambayo tulikuwa na bunge maalumu ambalo tulijadili katiba mpya ya Tanzania na ndani ya yale mapendekezo likaweko lile suala la hamsini kwa hamsini. Lakini pamoja na kwamba halijatoka kikatiba, utekelezaji unaendelea. Mimi nachukulia kwamba Tanzania tumepiga hatua kubwa. Kwa sababu kuwepo kwangu hapa kulianza na maamuzi ya makusudi kwamba kutekeleza ile hamsini kwa hamsini. Suala la 50/50 tulikuwa tulilisemea sana kwenye Bunge kwenda chini nafasi za madiwani na wengineo. Hivyo basi, mwaka 2015 serikali na Chama Cha Mapinduzi wakasema hapana hata juu kule tunakwenda 50/50 na ndio maana tukaamua ikiwa rais mwanaume, basi makamu wa rais atakuwa mwanamke, akiwa Spika mwanaume, Naibu Spika atakuwa mwanamke, na kinyume chake na pia nafasi nyingine. Sasa maamuzi yale ndiyo yaliyopelekea mimi kuwa Makamu wa rais wa kwanza mwanamke. Na katiba yetu inazungumza kwamba ikitokea sababu yoyote ile Rais akashindwa kufanya kazi zake labda kwa sababu ya kifo, kuugua au mambo mengine Makamu wa Rais atashika nafasi yake na ndivyo ilivyokuwa mimi nikawa niko hapo, kuwa Rais."

Pengo hili lilipelekea Msajili wa Vyama vya Siasa kubainisha suala la ushiriki wa wanawake katika uongozi kama shughuli mojawapo itakayoshughulikiwa na Kikosi Kazi, alichokiunda kushughulikia ujenzi na uimarishaji wa Demokrasia katika muktadha wa vyama vingi.

## 2.0 Kuundwa kwa Kikosi Kazi Na Suala la Ushiriki wa Wanawake Katika Siasa ya vyama Vingi.

Baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuonesha nia ya kuimarisha demokrasia shirikishi nchini kwa kufungua milango ya ushiriki wa vyama vingi katika ujenzi wa demokrasia, Msajili wa Vyama

vya Siasa, aliitisha Mkutano wa wadau wa Demokrasia ya Vyama Vingi tarehe 15 hadi 17 Desemba 2021 Jijini Dodoma. Mkutano huu ulijadili masuala ya msingi yanayohitajika katika ujenzi wa demokrasia ya vyama vingi. Washiriki walibainisha mapendekezo mengi kwa msajili yaliyohitajika kufanyiwa kazi ili kuimarisha demokrasia ya vyama vingi. Msajili wa Vyama vya Siasa, akaamua kuteua Kikosi Kazi cha kuchambua maoni ya wadau na kutoa mapendekezo yao kwa Rais wa Jamhuri Ya Muungano wa Tanzania. Kati ya maeneo tisa yaliyobainishwa ya kufanyiwa kazi, **ushiriki wa wanawake na makundi maalum** katika Siasa na Demokrasia ya Vyama Vingi lilikuwa moja wapo.

Katika mkutadha huu, Sisi Wanamtandao wa Wanawake Katiba, Uongozi na Uchaguzi, tumefanya uchambuzi yakinifu ya Mapendekezo ya Kikosi Kazi hususan mapendekezo yanayohusu ushiriki wa wanawake na makundi maalum katika demokrasia ya Vyama Vingi.

## 2.1 Mapendekezo ya Kikosi Kazi Kuhusu Ushiriki wa Wanawake Katika Uongozi.

Awali ya yote, Sisi Wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi, tunampongeza Msajili wa Vyama vya Siasa kwa kutambua uhusiano ulioko kati ya ujenzi wa Demokrasia na ushiriki wa wanawake, kwa kubainisha suala la urshiriki wa wanawake kama moja ya hadidu rejea za Kikosi Kazi kilichopewa jukumu la kuchambua, na kutoa mapendekezo yatakayo ongoza ujenzi wa demokrasia shirikiri kwenye muktadha wa vyama viangi Tanzania.

## 2.2. Uchambuzi wa Ripoti ya Kikosi Kazi kuhusu Demokrasia Ndani ya Vyama vya Sisasa, na Usawa wa Jinsia

Uchambuzi wa Ripoti ya Kikosi Kazi uilikiri kwamba, tangu kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi miaka 30 iliyopita, bado idadi kubwa ya vyama vya siasa vyenye usajili haviendeshwi kama taasisi na kwa kuzingatia misingi ya demokrasia. Jambo ambalo linasababisha manug'uniko mengi kutoka kwa wadau wengi ikiwa ni pamoja na malalamiko kuhusu **kutokuzingatia misingi ya usawa wa jinsia,** makundi maalum na kuthibiti viatendo vya unyanyasaji wa kijinsia. Sura ya Sita ya ripoti ya Kikosi Kazi, imeanza kwa kubainisha msingi ya usawa wa Jinsia katika Mikataba, Maagano, Matamko, na Makubaliano ya Kimataifa, Kikanda na Kikatiba kama tulivyoibanisha katika utangulizi kwenye Makala hii.

2.2.1 Tafsiri ya Dhana ya Makundi Maalum

**Katika Ripoti hii, Kikosi Kazi kilianza kwa kutoa tafsiri ya Kundi Maalum kwa kusema:**
***"Makundi maalum kwa muktadha wa kisiasa, demokrasia na uongozi nchini ni wanawake, wazee, vijana na watu wenye ulemavu"*** Ikumbukwe kwamba, kwenye hadidu rejea za kazi za Kikosi Kazi, walitakiwa kutoa uchambuzi na mapendekezo kuhusu Ushiriki wa Wanawake, na Makundi Maalum, hata hivyo, Kikosi Kazi kiliamua kuwaweka wanawake, ambao ni zaidi ya nusu ya Watanzania wote kwenye sanduku moja la "Makundi Maalum". Sote tunatambua kwamba,

kwenye kundi la wanawake, kama ilivyo wanaume, kuna wazee, watu wenye ulemavu, vijana, wanawake wenye uwezo wa uchumi, na wangine walio kwenye wimbi la umaskini wa kupindukia, wanataaluma, viongozi wa kisiasa, na wa taasisi mbalimbali, wenye elimu rasmi na wale ambao hawakubahatika kwenda shule kwenye mifumo rasmi. Makundi haya yote yana uhitaji tofauti katika muktadha wa demokrasi ya vyama vingi. Sisi wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi**, tuna kataa** tafsiri ya kikosi Kazi kuhusu Kundi Maalum, kwani haiendani na kazi waliyopewa kuhusu kushughulikia ushiriki wa agenda ya "Wanawake, na Makundi Maalum". Na kwamba tunaamini **kuwa** wanawake kwa ujumla wao siyo kundi maalum.

### 2.2 **Uchambuzi wa Kikosi Kazi Kuhusu Ushiriki wa Wanawake Katika Siasa ya Vyama Vingi.**

Baada ya kupitia kwenye ke storia ya ushiriki wa wanawake katika uongozi hapa nchini, Kikosi Kazi, kilibainisha maoni ya wadau mbalimbali kwenye suala hili, pamoja na kurejea kwenye mapendekezo ya Tume mbalimbali kuhusu suala hili.

#### 2.2.1. **Kuhusu Maoni ya wadau:**

**Kuhusu Viti Maalum:** Kikosi Kazi kilikiri kwamba, wadau wengi walipendekeza kufutwa kwa mfumo wa viti maalum kwa Wabunge, Wawakilishi na Madiwani kwa sababu zifuatazo:

(a) Unawanyima wanawake kuwa na haki ya kuwachagua wawakilishi wao, kwani haki ya kuwachagua wawakilishi imehodhiwa na Vyama vya Siasa na hivyo wateule wanakuwa wawakilishi wa vyama vya siasa badala ya kuwa wawakilishi wa wanawake.
(b) Unaendeleza mfumo kandamizi ambao wanawaake wabunge, wawakiishi na madiwani wa vitu maalum kuwa na hadhi tofauti na wale wa majimbo, kwani hawawezi kuteuliwa nafasi ya Waziri Mkuu, na hawapati fedha za Mfuko wa Jimbo.
(c) Kukosekana kwa mfumo maalum unaoongoza suala la utezi wa wawakilishi wa viti maalum na uongozi ndani ya Vyama vya Siasa.

Hivyo Basi, wadau walipendekeza:

(d) Kuzifanya Halmashauri/Manispaa kuwa Jimbo la Uchaguzi na kuwa na wagombea wawili wa kupigiwa kurua na wananchi, ambapo mmoja atakuwa ni mwanamke na mwingine mwanaume.
(e) Vile vile walipendekeza mfumo wa Viti Maalum vibakie kwa watu wenye kuishi na ulemavu na wale kumi wanaoteluliwa na Rais. Vile vile kuwa na Viti Maalum kwa Vyama vya Siasa ambavyo vimeshiriki uchaguzi mkuu na kufanikiwa kupata kiwango cha kura ngalau asili mia 5, ambavyo vitakuwa vya wanawake na wanaume ambapo viongozi wakuu wa vyama husika wateuliwa kuwa wabunge.
(f) Awepo mgombea huru katika ngazi ya ubunge na udiwani kwani uwepo wake kutafungua fursa kwa wanawake ambao si wanachama wa vyama vya siasa na ambao wanakubalika ndani ya jamii.

(g) Wadau walibainisha mazingira magumu yanayowakabili baadhi ya wanawake wanaoatia nia ya kugombea uongozi ndani ya Vyama vya Siasa, au kuomba kuteuliwa kuwa wagombe, ni pamoja na (i) unyanyapaa ndani ya vyama vya siasa, ambopo hushawisha kuongojea viti maalum. (ii) Vile vile, udhalilishaji wa maneno yenye kutweza utu wa mwanamka (iii) tatu ni kufanyiwa vitendo vya ukatili wa jinsia. Hivyo wadau walipendekeza kuweka kuwekwa kwa uwanda sawa wa wagombe kama njia ya kudumu ya kupunguza unyanyapaa wa wanawake, ili kuboresha ushiri wa wanawake katika ngazi za maamuzi.

(h) Wadau walikiri kwamba, ushiriki wa wanawake katika siasa, demokrasia na uongozi haujafikia malengo ya kitaifa, na kimataifa. Kwa mfano, idadi ya wanawake viongozi katika Vyama vya Siasa bado ni ndogo sana. Ili kuwa na usawa wa jinsia katika uchaguzi wa wabunge na madiwani ni vyema kuwa na ubunge na udiwani katika jimbo na kata, ambapo nafasi moja inakuwa kwa ajili ya mwanamke na nyingine mwanaume.

(i) Katiba za Vyama vya Siasa ziwe na ibara zinazoshughulikia masuala ya ukatili wa jinsia

(j) Kuwe na program shirikishi zitakayowajengea uwezo wanawake kugombe nafasi mbalimbali za uongozi

(k) Baraza la vyama vya siasa liongeze idadi ya wanawake ili kuweka uwiano ulio sawa.

(l) Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa iwe na dawati la jinsia litakalofanyia kazi masuala ya jinsia ndani ya Vyama vya Siasa.

(m) Sheria ya Vyama vya Siasa ifanyiwe marekebisho ili kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi za maamuzi ndani ya vyama ianze, na angalau 1/3 mpaka kufikia asili mia 50 kuwa na usawa wa jinsia kuanzia ngazi ya tawi mpaka Taifa. Aidha ivitake vyama vya Siasa kuwa na sera ya Jinsia na makundi maalum

(n) Kila Chama kiwe na Mpango Mkakati wa kufikia usawa wa kinjinsia.

(o) Ili kupata kwa urahisi usawa wa jinsia ni vyema ukaanzishwa mfumo wa uchaguzi wa uwiano kwa kura katika ubunge na udiwani (Proportional Representation)

(p) Kuwa na utaratibu wa kisheria utaoeleza kuwa katika uongozi wa vyama vya siasa, kuwe na usawa wa kijinsia, mfano, Mwenyekiti akiwa mwanamke Makamu Mwenyekiti awe Mwanaume;

(q) Kuhakikisha kuna uwazi ndani ya Vyama vya Siasa wakati wa uteuzi wa wagombea, ni muhimu sheria ya uchaguzi kujumuisha masuala ya jinsia katika miongozi ya kila chama kwa mujibu wa sheria

### 2.2.2 Mapendekezo ya Tume Mbalimbali:

Kwenye kurejea mapendekezo ya Tume mbalimbali, Kikosi Kazi kilitumia mapendekezo ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2013, iliyoongozwa na Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba**.** Tume hii ilipendekeza kupunguzwa kwa majimbo ya uchaguzi na kutengeneza mfumo utakaowezesha kila Chama cha Siasa kupendekeza wagombea wawili ambao watapigiwa kura na wananchi wa jimbo husika ambapo mmoja atakuwa mwanamke na mwingine mwanaume.

Vile vile misingi ya Usawa wa Jinsia, iliingizwa kwenye Katiba iliyopendekezwa ambayo Kikosi Kazi kilirejea. Kwa mfano, Ibara ya 6 (2)(g) ilikiri, Katiba inayopendekezwa ina -ainisha misingi ya utawala bora katika Jamhuri ya Muungano inayojumuisha Usawa wa Jinsia, ambapo Ibara ya 57, inaeleza kwamba, kila mwanamke ana haki sawa ya: (a) kuheshimiwa , kuthaminiwa, na kutambuliwa utu wake (b) kulindwa dhidi ya ubaguzi, udhalilishwaji,dhuluma, unyanysaji, ukatili wa kijinsia na mila potofu(c) Kushiriki bila ubaguzi katika uchaguzi na ngazi zote za maamuzi, (d) kupata fursa sawa na ujira sawa na mwanamme katika kazi zenye sifa zinazofananana kulindwa ajira yake wakati wa ujauzito na pale anapojifungua (f) kupata huduma bora ya afya ya uzazi salama na kumiliki mali. Vile vile Ibara ya 208 (1) (g) inaelezea kuwa, kuhakikisha kwamba uteuzi na ajira katika nafasi mbalimbali unazingatia uwezo, wa kitaaluma, weledi na maarifa, ujuzi na usawa wa jinsia, na uzoefu katika eneo husika na fursa sawa kwa watu wenye ulemavu.

Kimsingi mapendekezo ya Tume ya Mh. Jaji Warioba, haya kutofautiana na yale ya wadau yaliyoainishwa na Kikosi Kazi.

### 2.2.3 Uzoefu Wa Nchi Nyingine

Kwenye kutoa uzoefu wa nchi nyingine, Kikosi Kazi kilijikita zaidi kwenye kurejea vipengele mbalimbali vya katiba za nchi husika. Pamoja na kwamba, Katiba huwa zinaweka misingi elekezi, bila jitihada za kufasiri hizi Katiba kwenye sera na mikakati pamoja na kuonesha nia na utashi wa kisiasa wa kuleta mabadiliko, Katiba pekee haiwezi ikazalisha usawa wa jinsia. Kwa nchi ya Morroco iliyotajwa, Kikosi Kazi hakikuonesha hatua zilizochukuliwa na nchi ya Morocco katika kutafsiri misingi ya katiba. Huko Morrocco, Katiba ilifuatiwa na mabadiliko ya Sheria kadhaa za uchaguzi zilizobainisha kiwango cha uwakilishi, sayari na Sheria zilizoongeza kiwango cha fedha za umma zinazotumika kuwezesha wanawake kushiriki katika ngazi mbalimbali za uongozi. Kwa upande wa nchi ya Rwanda, iliyotolewa mfano, kuna mambo mengi yaliyochangia kuwezesha Rwanda kuvuka lengo la 50/50 ikiwa ni pamoja na ke storia ya ushiriki wa wanawake katika kujenga upya Rwanda iliyotokana na majeraha ya umwagaji damu, utashi wa kisiasa wa kutaka mabadiliko ya kimapinduzi katika uwanda wa siasa na uchechemuzi uliyofanywa na wanawake wenyewe. Mifano ya Kenya na Uganda haitupi mafunzo wezeshi kwani bado hawajafikia lengo la 50/50. Zipo nchi nyingine Barani Afrika na nje ya Bara hili ambazo zingaliweza kutupa mafunzo ya jitihada za Vyama vya Siasa na serikali katika kuongeza ushiriki wa wanawake bila kusababisha mifumo ya kibaguzi kama iliyoko sasa hivi kwa upande wa Viti Maalum nchini kwetu. [1]

Kwa maneno mengine, mifano ililyotolewa haikuonyesha maeneo ambayo sisi kama nchi tungaliweza kupata mafunzo kwenye kuongeza ushiriki wa wanawake katika nyanja zote za uongozi.

---

[1] Kwa mfano huko Nambia chama cha Swapo kilitumia mfumo wa hiari wa kuongeza ushiriki wa wanawake kwa njia waliyoita " punda mlia" kwenye teuzi za wanaowania nafasi ya uteuzi. Jambo ambalo liliongeza idadi ya wanawake katika chaguzi.

**2.3 Mapendekezo ya Kikosi Kazi kuhusu Ushiriki wa Wanawake katika Siasa na Uongozi**

Mapendekezo ya Kikosi Kazi kuhusu ushiriki wa wanawake katika siasa na uongozi hayakutokana kabisa na maoni ya wadau, wala yale yaliyotolewa na Tume ya Mh. Jaji Warioba. Vile vile hayakutokana na uchambuzi yakinifu ya mifano iliyotolewa kuhusu mikakati iliyotumiwa na nchi husika kuongeza ushiriki hususan nchi ya Rwanda ambayo ni nchi pekee iliyoweza kufikia zaidi ya 50/50 kutokana na mikakati madhubuti iliyochukuliwa na Serikali. Katika sehemu hii tutatoa mifano michache ambayo sisi Wanamtandao tunaihoji na kuikataa moja kwa moja.

**2.3.1. Kuhusu Viti Maalum**

Licha ya kwamba, wadau na Tume walishauri kuondolewa kwa mfumo wa Viti Maalum, Kikosi Kazi kiliamua Mfumo wa Viti Maalum uendelee bila kutoa sababu za msingi za kuendeleza huu mfumo wenye athari zilizoibuliwa na kutambuliwa na Kikosi Kazi katika uchambuzi wa maoni ya wadau. Vile vile Kikosi Kazi kilipendekeza kwamba, Wabunge wa Viti Maalum waitwe Wabunge wa Taifa na Madiwani waitwe Madiwani wa Wilaya. Vile vile Kikosi Kazi kilipendekeza Sheria ya Mfuko wa Uchaguzi ibadilishwe ili Wabunge wa Viti Maalum wafaidike nao kama Wabunge walioteuliwa kwa kupitia majimbo ya Uchaguzi. Na kwamba kuweko kwa mwongozo wa kisheria wa uteuzi wa wagombea na uchaguzi wa viongozi ndani ya Vyama vya Siasa ikiwemo wabunge wa Viti Maalum ili kusaidai uteuzi na uchaguzi wa haki na huru.

Kikosi Kazi kilidai kwamba, mfumo huu utumike "***kama njia ya kupata uzoefu na kisha kupisha wanawake wengine wenye nia ya kuongoza uzoefu na ujuzi wa masuala ya siasa"*** Kwa maneno mengine, Kikosi Kazi kinadai kwamba hata baada ya miaka zaidi ya 30 ya kuweko kwa Viti Maalum, bado wanawake wengi **hawana uzoefu, na ujuzi wa masuala ya kisasa.**

Kwetu sisi Wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi, tunaona pendekezo la kuendeleza Viti Maalum ambavyo sisi kama wadau tunaoathirika na mfumo huu wa ubaguzi ni kuendeleza **kutujengea imani** kwamba hatuna uwezo, uzoefu, wala ujuzi wa masuala ya siasa, na wengi wetu ikiwa ni pamoja na hao walioko kwenye uwanda wa siasa, tutahitaji takriban miaka kumi ya kujenga uwezo huo ili tuwapishe wenzetu wanaowania kuingia kwenye uwanda wa siasa. Fikra hizi ndizo zilizoelekeza tafsiri ya Kikosi Kazi kuhusu Makundi Maalum, kwa kuwabainisha wanawake wote kuwa wako kwenye kundi maalum katika muktadha wa Siasa na kutoa mapendekezo ambayo hayatokani na madai yetu sisi wadau, yaani sisi wanawake, na ambayo yanakinzana na dhamira za nadharia zilizoko kwenye katiba za vyama, na ilani zao ambazo zimebainisha nia na dhamira ya kujenga usawa wa jinsia.

Kwetu sisi pendekezo la kuendeleza mfumo wa Viti Maalum, ni la kuturudisha nyuma, na kwa kudharau, na kupuuza hazina ya ujuzi, ulioko miongoni wa wanawake wengi kwenye masuala ya siasa na uongozi. **Sababu zilizotolewa na sisi wadau za kuondolewa kwa mfumo huu wa viti maalumu bado ni halali na hatuta kubaliana kabisa na pendekezo la kuendeleza huu mfumo kandamizi na uliyowaondolea wanawake fursa katika uwanda wa ushindani katika nyanja**

**ya siasa**. Tatizo siyo kukosa uzoefu, wala ujuzi, tatizo ni kuwepo kwa vikwazo vingi na fikra mgando kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii yetu, ambazo zinaendeleza kuziba mianya mingi kwa wanawake pale wanapotia nia ya kuwania nafasi katika chaguzi mbalimbali**.**

### 2.3.2. Sheria ya Vyama vya Siasa Kurebishwa

**Kikosi Kazi kilielekeza mambo kadhaa yafanyike kwenye marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ili kuwezesha ushiriki wa wanawake katika ngazi zote za uongozi.**

**Mapendekezo hayo ni pamoja na:**

i) Kuweka sharti la kisheria kwamba idadi ya jinsi moja katika vyombo vya maamuzi isizidi asili mia 40. Kwa vyovyote idadi hii inahusu wanawake kwani hali halisi ya sasa ni takribani asili mia 99 ya uongozi ndani ya vyama vya siasa imehodhiwa na wanaume. Kiwango hiki cha asilimia 40 Kimepitwa na wakati, kwani kwa wale tuliyoshiriki kwenye mchakato wa utayarishaji wa Katiba Mpya, tutakumbuka kwamba, alilyekuwa mwenyekiti wa Kamati ya Uandishi Mh. Chenge, ilibainisha mfumo wa kufikia hamsini kwa hamsini kwa njia ya majimbo ya uchaguzi ambapo wajumbe wote, wanawake kwa wanaume watapigiwa kura kwa njia ya majimbo ya uchaguzi. Leo hii hatuwezi tukarudishwa nyuma na wachache wenye hofu ya kuweka mfumo linganifu katika uwanja wa ushindani kwa kisingizio cha kuwajengea wanawake uzoefu na ujuzi miaka zaidi ya sitini tangu tupate uhuru.

ii) **Kuweka sharti la kila Chama cha Siasa kuwa na sera ya jinsia**.

Hili ni Pendekezo zuri lakini tayari Vyama vingi hususan Vyama vikubwa, vina, sera, miongozo na matamko kwenye Katiba zao, miongozo na hata ilani zao kuhusu usawa wa jinsia. Kwa mfano, chama cha CCM kimetunga sera pana na sheria zinazoweka misingi ya usawa kitaifa, ikiwa ni pamoja na ushiriki katika mifumo yote ya maamuzi, kwa makundi mbalimbali. Ilani ya CCM ya Uchaguzi wa mwaka 2010 ilikiri kwamba kutokana na “ *uwezo na nguvu kubwa ya wanawake katika kusukuma kasi ya maendeleo na kuleta mageuzi ya uchumi, kijamii na kisiasa* (Ibara 176)—chama kilidhamiria kuongeza uwakilishi wake kutoka asili mia 30 kufikia asili mia 40. Na baadaye hii lengo likafikia 50/50 kwenye uchaguzi wa mwaka 2015.

Utangulizi wa Katiba ya CUF, inakiri kwamba “wanawake na wanaume wana haki ya kushiriki katika maamuzi yanayohusu maisha yao ya kisiasa, kiuchumi na kijamii bila ubaguzi kwa misingi ya jinsia au mila.” Kwenye alama za Chama, mizani yake inaashiria azma ya Chama ya kutoa haki sawa kwa wote. Kati ya malengo yaliyobainishwa kuna lengo la “kulinda haki za wanawake, wazee, walemavu na watoto kwa kuondoa hali yoyote ile inayowapuuza, inayowadhalilisha na inayowaonea” (Ibara ya 12). Vilevile kati ya haki za wanachama zilizobainishwa ni pamoja na haki ya kuchagua na kuchaguliwa katika uongozi (10:2). Marekebisho ya Katiba yaliyofanywa mwaka 2010, yameingiza mfumo wa uchaguzi unaoelekeza uwakilishi wa wanawake kuwa asilimia 30 katika ngazi zote.

Ilani ya chama cha CUF inakiri kwamba "**mfumo dume uliojikita katika kila nyanja ya maisha ni kikwazo cha maendeleo. Ili kukabiliana na mfumo huu, itaboresha mfumo wa sasa wa viti maalum ili kuongeza idadi ya wanawake katika ngazi zote za uongozi.** Hata hivyo njia za uboreshwaji hazikubainshwa

Halikadhalika, Katiba ya Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) imebainisha msingi wa usawa wa binadamu usiojali upendeleo au ukandamizaji wa kundi moja dhidi ya jingine kwa kujali rangi, jinsia, umri au itikadi. Sura ya Nne ya Katiba ya CHADEMA 2006 inabainisha msingi huu kwa kina. Ibara ya 4.1.1 inasema kuwa madhumuni ya kisiasa ya CHADEMA ni pamoja na "Kukuza, kulinda, kuelimisha na kutetea haki za binadamu katika misingi ya Tangazo la Ulimwengu la haki za Binadamu na Mikataba yote ya Kimataifa inayolinda haki hizo na inayofutilia mbali ukandamizaji wa watu katika misingi ya rangi, jinsia, ukanda, umri au itikadi." CHADEMA kinaamini katika "Kuendeleza na kudumisha Demokrasia katika mfumo wa vyama vingi vya siasa, kujenga utamaduni wa demokrasia katika jamii kwa kutambua haki za wengi katika maamuzi na pia kutambua haki za wachache kusikilizwa, kuheshimiwa na kulindwa, sambamba na kukubali ushindani huru, wa haki na wa wazi katika uchaguzi" (Ibara 4.1.3)."

Katiba ya NCCR-M ya mwaka 2002 inabainisha misingi ya Kisiasa na Madhumuni ya Chama. NCCR-M kinafuata itikadi ya demokrasia ya kijamii ambayo lengo lake ni ujenzi wa jamii yenye uhuru, haki za binadamu, usawa na ustawi wa jamii na inayokubali kutegemana kwa binadamu katika msingi wa mmoja kwa wote na wote kwa mmoja [Ibara 7(1)]. NCCR-M inaamini "Kuwa na jamii isiyo na ubaguzi wa rangi, kabila, dini au jinsia na kuhakikisha panakuwepo usawa na haki kijinsia kati ya wanawake na wanaumbe katika Nyanja zote za maisha" [Ibara 7 (13)].

Sera za Chama Cha NCCR- Mageuzi 2005 zinasisitiza kutokomeza aina zote za ubaguzi na ukandamizaji. Sera ya NCCR-M inatilia mkazo kuondosha ukandamizaji wa kihistoria kwa wanawake. Chama kinasema:

**"*Historia imembagua mwanamke, kumdharau na kumtweza. Hakupewa nafasi ya kujiendeleza kielimu, kiajira na katika kumiliki mali na uchumi wa familia na wa nchi. Mwanamke alidunishwa kwa vile tu yeye ni mwanamke. Ubaguzi huo wa kijinsia si halali na ni kashfa kubwa kwa binadamu. Lazima utamaduni mzima unaoshikilia dhana kwamba mwanamke ni kiumbe duni na dhaifu ubomolewe na kufutwa. Wanawake kama wanaume wana haki ya kuongoza kwenye fani zote ndani ya jamii".***

Kwa mifano hii michache, pendekezo la Kikosi Kazi kuhusu kuweko kwa sera za jinsia kwenye vyama, halikutokana na uchambuzi yakinifu wa sera ilani na matamko kuhusu ushiriki wa wanawake katika nyanja ya uongozi yaliyoko kwenye maandiko mbalimbali ya Vyama husika. Tatizo ni kutafsiri hizi sera, miongozo na Katiba za Vyama kwenye mikakati na vitendo vya dhati vya kufungua milango ili wanawake washiriki katika uongozi wa Vyama vyenyewe na kuteuliwa kwenye kuwania nafasi za uongozi. Tatizo kubwa ni mfumo dume kama moja ya sera za Vyama

ilivyokiri. Hii inajidhihira na takwimu za uteuzi wa wanawake katika kuwania uongozi pamoja na nafasi za wanawake katika uongozi ndani ya vyama vyao ikiwa ni pamoja na vile vyama vilivyokiri nia ya kubomoa mfumo dume.

Kwa mfano, Ingawaje wanawake wapiga kura walikuwa asili 53%  katika Uchaguzi wa mwaka 2015, vyama vilivyoshiriki katika uchaguzi viliwateua wanawake kama ifuatavyo:

- **Waliogombea viti vya urais:** 8 waliyoteuliwa na Vyama vyao katika ngazi ya awali walikuwa 3, na kuteuliwa kuwa wagombea ni 1 kati ya wagombea 8 wa nafasi hizo.
- **Walioteuliwa kugombea nafasi za ubunge:** Kati ya wagombea 1,250 wa viti vya ubunge waliyoteuliwa na vyama vyao kugombea nafasi hizi ni 238 ( 19% tu).
  - CCM asili mia 9%
  - Chadema asili mia 6%,
  - ACT  Wazalendo asili mia 15%
  - CUF asili mia 11%
- Wagombea nafasi za udiwani: kati ya 10,879 waliyogombea nafasi hizi wanawake walikuw 679 tu ( 6.2%)

Hii taswira ina maanisha kwamba, hakuna Chama kilichotafsiri sera, liani na hata Katiba zao katika kufungua milango ya ushiriki wa wanawake katika uchaguzi wa mwaka 2015.

**Uchaguzi wa 2020 hali haikubadilika sana**

Katika uchaguzi huu, jumla ya wagombea 1,257 waliteuliwa na wasimamizi wa uchaguzi kugombea nafasi za ubunge katika majimbo 264. Kati yao wanawake walikuwa 293 sawa na asili mia 23 tu na wanaume 964  sawa na asili mia 77. Kwenye teuzi hizi, Chama Cha Mapinduzi kilikuwa na jumla ya wagombea 264, kiliteua wanawake 25 tu na wanaume 239. Chama cha CHADEMA, kilikuwa na wagombea 211, kiliteua wanawake 58, na wanaume 153. Chama cha ACT Wazalendo, kilikkuwa na wagombea 156, kiliteua wanawake 21 na wanaume135. Chama cha CUF, kilikukwa na wagombea 154, kikateua wanawake 38, na wanaume 116.

Teuzi hizi haziendani na dhamira zlizooneshwa na Vyama hivi vya Siasa katika Katiba zao, Ilani zao wala mipango mikakati yao. Hili ndilo tatizo ambalo Kikosi Kazi kingeshughulikia badala ya kupendekeza kuweko kwa Katiba, au sera ambazo tayari ziko. Kwetu sisi Wanamtandao wa Wanawake, Katiba Uongozi, na Uchaguzi, Kikosi Kazi haki kuonyesha umakini kwenye kuchambua mizizi ya tatizo la kutoshiriki kwa wanawake katika siasa na uongozi. Kwetu sisi Wanamtandao huu, tatizo kubwa ni kukosekana kwa utashi wa siasa wa kubomoa mfumo dume unaoongoza fikra na itikadi za utendaji wa Vyama vya Siasa ambavyo Sheria za Vyama na za uchaguzi zimewapa mamlaka ya kufunga na kufungua milango ya ushiriki wa wanawake katika siasa na uongozi wa vyama na wa nchi yetu

### 2.3.3 Kuhusu kuweko Pendekezo la Kuwa na Dawati la Jinsia Kwenye Ofisi ya Msajili na Kila Chama cha Siasa.

Tangu Mkutano wa Beijing mwaka 1995, Serikali imeanzisha madawati ya Jinsia katika Wizara na Taasisi mbalimbali za umma ili ziweze kushughulikia masua ya jinsia pamoja na kufuatilia utendaji. Pale ambapo vitengo au madawati haya yamepewa vitendea kazi, na kupewa mamlaka wezeshi ya kutenda kazi hasa kwenye kusaidia kuingiza masuala ya jinsia kwenye sekta na taasisi husika, basi kumekuweko na matokeo chanya. Lakini mara nyingi chambuzi zinaonesha kwamba vitengo hivi havina vitendea kazi, rasilimali pamoja na ujuzi wa kuweza kufanya kile walichotakiwa kufanya. Hivyo Pendekezo la kuwa na madawati ni kitu kimoja, sayari na pendekezo hili sharti vitengo hivi viwezeshwe kufanya kazi na kupewa hadidu rejea zinazoeleweka.

**2.3.4. Kuhusu Idadi ya Wanawake Katika Baraza la Vyama vya Siasa.**

Kikosi Kazi kwa kutambua kwamba, uongozi wa juu wa Vyama umehodhiwa na wanaume, walipendekeza kuteuliwa wanawake kutoka Vyama vya Siasa, angalau wawili wawili ili kuongeza idadi hiyo. Pendekezo hili lingekuwa ni la muda mfupi ili mikakati ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika uongozi wa Vyama ufanyiwe kazi kisheria.

**2.3.5 Kuhusu maboresho ya Sheria ya Mfuko wa Jimbo**

Kikosi Kazi kilipendekeza maboresho ya Mfuko wa Jimbo ili Wabunge wa Viti Maalum wanufaike nao. Pendekezo la Wanamtandao la Kuondoa mfumo wa Viti Maalum hailazimu mabadiliko ya Sheria ya Mfuko wa Jimbo kwa vile kila Mbunge atakuwa na hadhi sawa na stahiki sawa.

**2.3.6. Kuhusu kuwa na Mgombea Huru.**

Kikosi Kazi kilipendekeza mabadiliko ya Sheria za Uchaguzi ili kuwe na mgombea huru. Hii inatoa fursa kwa wanawake ambao hawana chama chochote lakini wenye kukubalika na jamii kuwania nafasi katika chaguzi. **Pendekezo hili tunaliunga mkono.**

**2.3.7. Kuhusu Kuundwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi**

Kikosi Kazi kilipendekeza kuundwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi kama mkakati mojawapo wa kuimarisha demokrasia ya Vyama Vingi hapa nchini. Sisi Wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi, **tunakubaliana na pendekezo hili**, lakini tuna maoni kuhusu mapendekezo ya mchakato na kuundwa kwa Tume yenyewe., kama inavyoonekana hapo chini

Kikosi Kazi kinapendekeza kuwa utaratibu ufuatao utumike kuwapata wajumbe wa tume ya Taifa ya Uchaguzi:

1. kuwe na Kamati ya Uteuzi ya Wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi itakayokuwa na wajumbe wafuatao:
    1. Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye atakuwa ni Mwenyekiti;
    2. Jaji Mkuu wa Zanzibar ambaye atakuwa Makamu Mwenyekiti;
    3. Kamishna wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Tanzania Bara;
    4. Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Zanzibar;
    5. Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu; na
    6. wajumbe wengine wawili watakaoteuliwa na Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baada ya kupendekezwa na Chama cha Wanasheria Tanganyika na Chama cha Wanasheria Zanzibar.
    7. Angalau wajumbe wawili wa Kamati ya Uteuzi wawe wanawake**;**

Kwa kutambua kwamba, wahusika kwenye hii kamati wengi wao watakuwa wanaume, Kikosi Kazi kilipendekeza, ngalau kuwe na wanawake wawili. Hakuna mwongozo jinsi ya upatikanaji wa Wanawake, na hakuna uwakilishi wa asasi za kirahia kwenye hili kundi

### 2.3 .8 Kuundwa kwa Tume Huru Ya Uchaguzi.

Kikosi kazi kilipendekeza kuweko kwa Mwenyeti, Makamu Mwenyekiti na Mjumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na kwamba sifa zao ziainishwe. Na kwamba kila Mtanzania mwenye sifa ana haki ya kuwakilisha maombi yake kwa Tume ya Uchaguzi. Kwenye hili, Kikosi Kazi kimekuwa kimya kuhusu uwakilishi wa wanawake. Sisi Wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi tunapendekeza kuzingatiwa kwa msingi wa 50/50 katika uundwaji wa Tume Huru ya Uchaguzi.

## 3.0 HITIMISHO

Kwetu sisi Wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uchaguzi na Uongozizi, hatukuridhishwa na mapendekezo yaliyotolewa na Kikosi Kazi kuhusu Ushiriki wa Wanawake katika siasa na uongozi katika muktadha wa siasa ya vyama vingi. Kwanza, mapendekezo hayakuchukua maoni yetu kama wadau wakuu katika mchakato wa kujenga demokrasia shirikishi wala ya Tume iliyosimamia mchakato wa kutayarisha Katiba Mpya. Vile vile mapendekezo ya Kikosi Kazi katika eneo hili hayakutokana na uchambuzi wa hali halisi hususan vizingiti na vikwazo vinavyokabili wanawake wanaponuia kuingia kwenye uwanda wa siasa ya ushindani.

Hivyo kwa maoni yetu, mapendekezo ya Kikosi Kazi yalilenga kuendeleza mfumo kandamizi na wa ubaguzi uliyowaondolea wanawake fursa ya kutumia vipaji, ujuzi na uzoefu wao katika masuala ya siasa na uongozi.

Vile vile mapendekezo haya, hayakutia maanani athari za kuendeleza mfumo wa Viti Maalum kwenye ujenzi wa demokrasia shirikishi, hususan katika kipindi hiki ambacho Rais mwanamke ameonyesha nia ya kufungua milango na vizingiti kwa Vyama vya Siasa na kuonyesha nia ya kupanua fursa za wanawake katika uongozi wa taifa letu.

Kutokana na hali hii, sisi Wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi tunadai mambo yafuatayo kuhusu ushiriki wetu katika demokrasia ya vyama vingi.

**4.0 Madai ya Wanamtandao Kuhusu Ushiriki wa Wanawake Katika Demokrasia ya Vyama Vingi.**

1. Sisi Wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi tumefanya uchambuzi yakinifu na wa kijinsia kuhusu mapendekezo ya kikosi kazi hususan mapendekezo yao kuhusu ushiriki wa Wanawake katika Uongozi na kwa sauti moja**, tunatamka kwamba, mapendekezo ya Kikosi Kazi kwenye eneo hili hayakutokana na maoni yetu kama taarifa yao inavyokiri, na wala kutokana na hali halisi ya ushiriki wanawake katika uongozi kama ripoti yao ilivyoainisha.** Kwa umoja wetu **tunakataa** pendekezo la kuendeleza mfumo wa Viti Maalum kwa sababu zilizobainishwa na Kikosi Kazi kutoka kwetu wadau na kupuuzwa kwenye mapendekezo yao.
2. Kwa pamoja tunapendekeza kwamba **mfumo wa kuwa na wagombea wawili kila jimbo la uchaguzi uzingatiwe ili kufikia 50/50** kama tulivyopendekeza katika madai yetu kwa Tume ya Warioba
3. **Vile vile Sisi Wanamtandao tunakataa kuingizwa kwenye kapu moja la " kundi Maalum" kwani sisi ni raia na ndani yetu kama lilivyo kundi la wanaume, kuna makundi maalum.**
4. **Tunakubaliana na pendekezo la kuundwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi,** lakini **tunapendekeza uundwaji wa Tume Hii uzingatia usawa wa Jinsia**.
5. Tunadai, **Sheria ya Vyama vya Siasa ibadilishwe ili kuwajibisha Vyama Vya Siasa kuzingatia msingi wa usawa katika ngazi zote za Uongozi ndani ya vyama na katika teuzi za vyama kwa wanaowania nafasi katika chaguzi za ngazi zote** .
6. Tunatoa **Wito** kwa wanawake wote na kwa wale wote wenye **kutetea haki za binadamu hususan haki za wanawake kuendelea kujenga nguvu ya pamoja ili kushinikiza ushiriki wetu kwa kuzingatia 50/50.**